# LEARNING BY EAR 2011

## “The Promised Land - A Story of African Migration to Europe”

## EPISODE SEVEN: “Survival in the Concrete Jungle”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann**

**KISUAHELI: Eric Ponda**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: LINDA AND FLORENCE AT A SHOPPING CENTRE**

- **Linda (f, 20)**
- **Florence (f, 35)**

**SCENE TWO: MR. MARAGA RETURNS HOME AFTER BEING LAID OFF WORK**

- **Mr. Maraga (m, 60)**
- **Mrs. Maraga (f, 55)**

**SCENE THREE: LINDA AND FLORENCE AT A FAST FOOD RESTAURANT**

- **Linda (f, 20)**
- **Florence (f, 35)**

**INTRO:**

Hujambo msikilizaji na karibu kwenye sehemu ya saba ya mfululizo wa mchezo huu wa Redio Noa Bongo Jenga maisha yako, tukiwa bado kwenye hadithi **“Ardhi ya Ahadi – kuhusu Wa-Afrika wanaohamia Ulaya.”** Katika kipindi kilichotangulia Sule anashangaa kumuona rafiki yake Farahani akiangaziwa katika vyombo vya habari kwenye taarifa kuhusu wahamiaji haramu waliokamatwa baharini na maofisa usalama wa mipaka ya Ulaya na kurejeshwa nyumbani. Upande mwingine, ni miezi minne sasa tangu Linda aanze masomo yake ya chuo kikuu huko Ulaya, ambako anakumbana na ukweli wa mambo halisi kuhusu maisha ya Ulaya. Amewasiliana na mchumba wake Chivasi, lakini akamdanganya kuhusu ugumu wa maisha anayopitia nchini humo. Hatimaye, Linda anampigia simu rafiki yake Florence, waliokutana kwa mara ya kwanza kwenye ndege wakiwa safarini kuelekea Ulaya. Anamuelezea matatizo yake ya kifedha. Je ni nini kitakachojiri leo? Endelea kuwa nasi hadi mwisho wa kipindi kwenye sehemu hii ya saba, **“Maisha jangwani.”** ambapo tunaanza na Linda na Florence wakikutana nje ya duka kubwa kwenda kumnunulia Linda nguo za kumkinga na baridi.

**SCENE ONE: LINDA AND FLORENCE OUTSIDE A SHOPPING CENTRE**

1. **SFX: Atmo street**

2. **LINDA:** Flo, sijui niseme nini! Nakushuru sana kukubali ombi langu japo kwa notisi ya muda mfupi. Nilikuwa napatwa na wazimu. Nilijihisi mpweke na rafiki yangu aliyesalia ni kitabu tu….!

3. **FLORENCE:** Linda, hilo si tatizo. Msichana mrembo kama wewe anahitaji kujipa raha japo mara moja moja. Tunaweza kwenda?

4. **SFX: HUGE SLIDING DOORS OPEN / ATMO SHOPPING CENTRE**

5. **LINDA:** **(awed by size of mall and range of products)** Wow! Pamependeza! Maduka mengi na tena yote katika jingo moja…Kisha kuna vitu vingi vizuri vizuri…..Haya ndiyo ninayoyasoma tu katika majarida ya masuala ya urembo, sivyo?

6. **FLORENCE:** **(happily)** Hahaha – unachekesha. Sawa twende basi nataka kukugeuza na kuwa Mwafrika Mzungu.

7. **LINDA:** Florence, nikuulize ? Lakini ni swali la kibinafasi?

8. **FLORENCE:** Uliza!

9. **LINDA:** Ulifikaje hapa? Yaani hapa Ulaya? Ulikuja kusoma? Au kufanya kazi? Unaendelea vizuri sana. Natamani ningekuwa wewe.

**10. FLORENCE:** Sawa, Linda. Jambo la kwanza usimuulize mhamiaji hasa kutoka barani Afrika alivyofika Ulaya. Ni mwiko katika utamaduni wa Mwafrika. Pili usijilaumu, pia wewe unaweza kuwa na vitu hivi nilivyonavyo. Lakini ni lazima uwe mtu wa subra na kujitolea maishani.

**11. LINDA:** **(curious)** Kweli ? Yaani kuwa na gari kama lako? Nguo, na mapambo ya urembo kama yako? Lakini kwanza lazima niajiriwe kama wewe!

**12. FLORENCE:** **(embarrassed)** Mmm!… Mambo kama hayo! Bado wewe ni mdogo. Sasa tunaweza kuondoka.

**13. LINDA:** Eti mimi bado mdogo! Basi nisingekuwa hapa Ulaya. Natimiza miaka 21 hivi karibuni. Sasa nimekuwa mtu mzima kufanya maamuzi mwenyewe. Napasa kujitolea vipi?

**14. FLORENCE:** Linda – Wahenga walisema maisha ya jangwa yanakutikana, barani Afrika, Asia na Marekani Kusini. Lakini hata hapa Ulaya pia ni jangwani .Tofauti ni kwamba huu ni mwamba wa jangwa lenyewe lakini sheria za jangwani ni zile zile na lazima uwe timamu! Hapa wahamiaji wanajikakamua zaidi kuliko wenyeji ili waweze kujimudu kimaisha… Unalipenda rinda hili?

15. **LINDA:** **(excited)** Ndiyo….linapendeza kweli!. Lakini …

16. **FLORENCE:** Nenda ukalijaribu kama litakutosha. Likikutosha nitakununulia

17. **LINDA:** **(disbelief)** Usinitanie! Sawa asante sana Flo, Asante- sijapata rafiki mzuri kama wewe….!

18. **NARRATOR:** Ukarimu wa Florence kwa Linda ni mwingi na umeanza kutia shaka, au unafikiriaje? Isitoshe wamekutana siku chache tu zilizopita. Ni nini hasa anachotaka kutoka kwa Linda. Linda anajaribu rinda lake, viatu, na koti moja baada la jingine. Florence anasema atagharamia mavazi hayo. Lakini wakati Linda anapokusanya bidhaa zake dukani, wazazi wake wanapata habari za kushtua. Hebu tuungane nao wanapowasili nyumbani.

**<u>SCENE TWO: THE MARAGAS RETURN HOME AFTER BEING LAID OFF</u>**

19. **SFX: DOG BARKING LIGHTLY**

20. **MR. MARAGA:** **(angrily)** Nyamaza wewe mbwa mpumbavu ! Huna habari ya mambo yaliyotukuta.

21. **MRS. MARAGA:** Ehh samahani, Mbwa hahusiki kwa vyovyote na sisi kufutwa kazi . Usimulimbikizie machungu!

22. **SFX: METAL DOOR BEING LOCKED**

23. **MR. MARAGA** **(bitterly)** Miaka 30-…. miaka 30 tumekuwa

tukifanya kazi kama watumishi wa umma, na kisha ghafla tunaambia hakuna kazi?, Ehh Mama Linda ni haki kweli hiyo?

**24. MRS. MARAGA:** Umemsikia vizuri mkurugenzi. Amesema kuwa hali hii inakumba ulimwengu mzima. Watu wanaachishwa kazi kila mahali. Usijali mpenzi, tutafaulu tu!

**25. MR. MARAGA:** **(still bitter)** Vipi tutaweza kukabiliana na maisha? Na ni kwanini watu wa ngazi za chini ndio wanaoathirika kila mara hali hii inapotokea? Hii ni haki kweli? Haiwezekani mke wangu! Hatustahili kufanyiwa mambo haya.

**26. MRS. MARAGA:** Keti basi mpenzi wangu. Nikutengenezee kikombe cha chai…! Utajisikia vizuri.

**27. MR. MARAGA:** **(with rage)** Sitaki hata kikombe cha chai! Kikombe cha chai kitanisaidia nini mimi? Ninachotaka ni kurejeshewa kazini!

**28. MRS. MARAGA:** Mpenzi, najua unapitia kipindi kigumu. Mimi pia hali ni hiyo hiyo. Lakini kumfokea mbwa kutasaidia nini? Hebu kwanza tutulie kisha tutapata jibu. Je ungependa nimweleze Linda mambo haya?

**29. MR. MARAGA:** Brenda, unawazimu? Unataka kumweleza nini

Linda? Kwamba wazazi wake wamefutwa kazi? Na hivi karibuni watapoteza makao yao pia? Unafahamu vyema kwamba ndio mwanzo binti yetu ameanza masomo yake. Unataka kumtia wasi wasi? Isitoshe hana habari kwamba hatutaweza kumlipia karo kwa miaka iliyosalia chuoni. Hakuna haja ya kumueleza!

**30. MRS. MARAGA:** **(calmly)** Maraga, sidhani kama hilo ni jambo la busara. Linda ni binti yetu, ndio mtoto wa pekee katika nyumba hii. Na anahitaji kufahamu yote yanayoendelea hapa nyumbani. Yeye ni mtu mzima kuelewa mambo haya, na kuweza kujimudu kwa hali yoyote ile, pengine anaweza kutusaidia.

**31. MR. MARAGA:** **(curious)** Kutusaidia? Kutusaidia vipi?

**32. MRS. MARAGA:** Kifedha! Nasikia wanafunzi wengi wa Kiafrika wanaoishi Ulaya hufanya kazi wakati wa muda wa wa ziada. Kwanini Linda asiweze kufanya hivyo? Ni kweli tunahitaji msaada wa kifedha, kwasababu hatuna mishahara na tayari tumetumia akiba yetu kugharamia masomo ya Linda.

**33. MR. MARAGA:** **(thoughtful)** Mmm… Kwa hivyo mtu anaweza kufanya kazi huko Ulaya huku akiendelea na masomo yake?

**34. MRS. MARAGA:** Hayo ndiyo niliyoyasema sasa hivi…

35. **MR. MARAGA:** **(irritated)** Najua umesema haya sasa hivi. Na kwanini hukuniambia mapema? Je! Linda anafahamu kwamba anaweza kufanya hivyo?

36. **MRS. MARAGA:** Kama hakuyajua haya kabla hajasafiri, nina hakika anayafahamu sasa. Kwanza nitashangaa sana nikisikia hajapata kazi hadi kufikia sasa katika mgahawa wao wa chuoni au mahali kwingineko.

37. **MR. MARAGA:** **(fondly)** Ni kweli. Linda anapenda sana kupika. Nadhani kile kikombe cha chai ni wazo zuri sana, nafikiri kitanisaidia sana.

38. **MRS. MARAGA:** **(jokingly)** Kama kawaida mimi huwa na mawazo mazuri. Subiri kidogo!

39. **NARRATOR:** Mtu yoyote aliyefutwa kazi, hapana shaka atakueleza sio tu ni pigo la kifedha bali la kifikra pia. Kwa bahati nzuri familia hii ya Mzee Maraga inajivunia kuwa na mtoto wao aliyeko Ulaya, ambaye anaweza kuwasaidia kifedha mara kwa mara. Tukirejea dukani, Florence tayari amelipia bidhaa za Linda na sasa wanaingia katika mgahawa mmoja kupata chakula.

## SCENE THREE: LINDA AND FLORENCE IN A FAST FOOD RESTAURANT

**40. SFX: FAST FOOD RESTAURANT ATMO**

**41. LINDA:** **(enjoying)** Kuku huyu ni mtamu! Flo, hakika hii ndiyo siku yangu ya kwanza ambayo nimeifurahia tangu niwasili Ulaya. Ningependa sana kuishi maisha haya. Niko tayari kufanya chochote kutimiza haya.

**42. FLORENCE:** Linda una hakika? Unafahamu kwamba pindi unapo fanya uamuzi hakuna kurudi nyuma.

**43. LINDA:** Rinda zuri, viatu vizuri koti kisha chakula kitamu... Naweza kurudi nyuma kweli? **(impatient)** Hebu niambie nifanye nini?

**44. FLORENCE:** Na mchumba wako Je?

**45. LINDA:** Nani? Chivasi? Ana nini?

**46. FLORENCE:** Ndio Chivasi – Unamweka wapi katika mipango yako?

**47. LINDA:** **(short silence)** Kusema kweli… eeeeh…hayupo mahali popote. Namaanisha bado nampenda tu, lakini kwanza lazima nijipange na maisha yangu hapa Ulaya. Yeye ana maisha yake huko nyumbani.

**48. FLORENCE:** Mna mipango ya kuoana?

**49. LINDA:** **(surprised) N**dio tuna mipango ya kuoana. Lakini hiyo ni baada ya mimi kukamilisha masomo yangu. Lakini kwa sasa nataka kufurahia maisha hapa Ulaya na kuishi kama wengine.

**50. FLORENCE:** Unaweza kuwa msiri Linda?

**51. LINDA:** Naweza.

**52. FLORENCE:** Yaani kuhifadhi siri, na kutomwambia mtu yeyote

**53. LINDA:** **(suspicious)** Hata wazazi wangu?

**54. FLORENCE:** Ndiyo wazazi wako. Na hata Chivasi pia.

**55. LINDA:** **(bit nervous)** Sawa…lakini sasa nimeanza kushikwa na wasi wasi! Kwani ni siri gani hiyo? Unauza mihadarati?

**56. FLORENCE:** Hapana! Hapana! Kwani ungependa kushirikiana na mtu anayejihusisha na mihadarati?

**57. LINDA:** Hapana, kabla ya kuwasili huku, nilikuwa nimeonywa kwamba mihadarati ni tatizo kubwa Ulaya. Hata miongoni mwa wanafunzi chuoni

mwetu.

58. **FLORENCE:** Hapana Linda, mimi sihusiki na mihadarati wala kuhusiana na walanguzi wa mihadarati.

59. **LINDA:** Sasa ni siri gani hiyo? …Ukahaba?

**(PAUSE)**

60. **FLORENCE:** Nikisema ndiyo utakubali?

61. **LINDA:** Nitasema: **(acts it)** “Florence, nashukuru sana kukutana na wewe, kwa muda wako na pia kwa ukarimu wako wa kuninulia zawadi, lakini samahani sikuja Ulaya kuuza mwili wangu.”

62. **FLORENCE:** Kweli unasema hivyo?

63. **LINDA:** Ndiyo. Kuna mambo naweza kuyakubali, lakini siwezi kushusha au kudunisha hadhi yangu – Hilo siwezi kuthubutu kulifanya.

64. **FLORENCE:** Lakini umesema kuwa uko tayari kuhifadhi siri? Sivyo?

65. **LINDA:** Ni kweli, naweza. Ilimradi tu si jambo la kunidhuru na wale ninaowapenda.

66. **FLORENCE:** Sawa Linda! Unasema unataka kuishi maisha

mazuri kama mimi? Na kwamba uko tayari kufanya chochote? Sasa kuna mpango nataka kukwambia.

**OUTRO:**

Je ni mipango gani Florence anataka kupendekeza kwa Linda? Na Linda atalichukuliaje pendekezo hili? Na rafiki zetu Farahani na Sule kutoka Afrika Kaskazini nao wanaendeleaje? Unawakumbuka? Ni miezi minne sasa tangu Farahani anusurike kufa maji baharini akijaribu kuvuka na kuingia Ulaya bila hati za kusafiria. Je wanapanga jaribio jingine? Au Sule amepoteza subira dhidi ya Farahani na ndoto yake ya kuhamia Ulaya? Usikose kusikiliza kipindi kinachofuata kwenye mchezo huu wa Ardhi ya Ahadi kuhusu Waafrika wanaohamia Ulaya, kutoa hoja zako kuhusu utaratibu unaopasa kufuatwa na Waafrika ili kuruhusiwa kuishi Ulaya. Pia unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kupitia mtandao wetu wa dw-.de/destinationeurope. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa..